



MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na. 11. Msimu wa Kilimo 2021/22


Tathmini, Januari 1-10, 2022 na Matazamio kwa Kipindi cha Januari 11-20, 2022

MUHTASARI

- Shughuli za kilimo zimeathiriwa na unyeshaji hafifu pamoja na kuchelewa kuanza kwa misimu ya mvua katika maeneo mengi nchini
- Hali ya ukavu iliyoonekana katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua za vuli imeathiri mazao yaliyopandwa mapema
- Wakulima wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani kutoka katika maeneo yao na kuchukua hatua stahiki katika shughuli zao za kilimo.
- Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani husika ili kudhibiti magonjwa ya mifugo na athari nyingine zitokanazo na hali ya hewa inayotarajiwa.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 1-10, 2022

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimaimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) ikipungua nguvu. Hali hii iliruhusu ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika baadhi ya maeneo nchini hususani upande wa magharibi, nyanda za juu kusini magharibi pamoja na maeneo ya kusini na hivyo kusababisha maeneo haya kupata mvua zilizoambatana na vipindi vya ngurumo za radi. Joto la bahari upande wa mashariki mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani wakati kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la juu kidogo ya wastani. Kwa ujumla mifumo hii ya hali ya hewa iliendelea kusababisha mvua zilizoambatanana ngurumo katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, nyanda za juu kusini magharibi na magharibi mwa nchi.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Januari 1-10, 2022. Chanzo cha data: data za vituoni na satelaiti (CPC Global Daily Unified Gauge-Based).

TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 1-10, 2022

Katika dikadi hii, baadhi ya maeneo nchini yalipata mvua kati ya mm 10 hadi mm 110 isipokuwa maeneno mengi ya mikoa ya Arusha, Manyara, Kigoma, Dodoma, Kilimanjaro, Tanga, north Morogoro, Pwani, Dar es Salaam pamoja na visiwa vya unguja na Pemba ambayo yalipata chini ya mm 10. Maeneo mengi ya mkoa wa Ruvuma yamepata mvua zaidi ya mm 110 kama inavyoonekana katika kielelezo.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 1-10, 2022

Katika kipindi hiki, mvua zilizonyesha katika maeneo yanayopata mvua za msimu zimesaidia shughuli za uandaaji wa mashamba na upandaji wa mazao. Wakulima wengi wamendelea na uandaaji wa mashamba na upandaji wa mazao. Zao la mahindi lipo kati ya hatua ya kuota na jani la tatu katika maeneo mengi yaliyopandwa. Mahindi yaliyopandwa mapema hususan katika mikoa ya Tabora, Katavi na Rukwa yapo katika hatua ya jani la tisa na baadhi ya wakulima wameanza palizi ya kwanza.

Kwa maeneo yanayopata mvua za vuli mvua zilizonyesha zimesaidia ukuaji wa mazao na malisho ya wanyama. Baadhi ya wakulima katika maeneo haya waliendelea na shughuli za upandaji na palizi. Wakulima katika mkoa wa Kagera waliendelea na shughuli za uvunaji maharagwe wakati huo mahindi yapo katika hatua ya kukomaa. Hali ya ukavu iliyoonekana katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua za **Vuli** imeathiri mazao yaliyopandwa mapema. Kwa ujumla shughuli za kilimo zimeathiriwa na unyeshaji hafifu pamoja na kuchelewa kwa misimu ya mvua katika maeneo mengi nchini. Maji na malisho ya mifugo na wanyamapori viliendelea kuongezeka kidogo katika maeneo mengi ya nchi.

HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2022

Kwa ujumla hali ya maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji kwenye mito viliendelea kuongezeka kidogo isipokuwa katika bonde la mto Rufiji na Ruvuma.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2022

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kupungua nguvu na na kuruhusu ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika maeneo ya magharibi, nyanda za juu kusini magharibi na kusini huku ikichagiza upatikanaji wa mvua zitakazoambatana na ngurumo katika maneo haya. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa upande wa mashariki mwa bahari ya Hindi na upande wa kusini magharibi mwa bahari ya Hindi kunatarajiwa kuwa na joto la juu ya wastani. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa upande wa kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi yetu. Kwa ujumla mifumo hii ya hali ya hewa inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa wa mvua zitakazoambatana na ngurumo kwa baadhi ya maeneo ya magharibi, nyanda za juu kusini-magharibi, kusini pamoja na ukanda wa Ziwa Victoria.

HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2022

Maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara)

yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo hususani katika nusu ya pili ya dekad.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) pamoja na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) pamoja na pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa katika maeneo ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) hususani katika nusu ya pili ya dekad.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) pamoja na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2022

Mvuua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitaendelea kuimarisha unyevunyevu kwenye udongo na hivyo kusaidia ukuaji wa mazao. Mvua zinazotarajiwa kunyesha katika maeneo yanayopata mvua za vuli ni za nje ya msimu na zinaweza kuathiri uvunaji na ukaushaji wa mazao hususan maharagwe.

Kwa upande wa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka wakulima wanashauriwa kuendelea na shughuli za upandaji kutegemea hali ya unyevunyevu kwenye udongo.

Wakulima wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani kutoka katika maeneo yao na kuchukua hatua stahiki katika kutunza mashamba na matumizi ya pembejeo kama vile mbolea na viuatilifu. Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani husika ili kudhibiti magonjwa ya mifugo na athari nyingine zitokanazo na hali ya hewa inayotarajiwa.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2022

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka katika maeneo mengi yanayopata mvua za msimu. Hata hivyo watumiaji rasilimali maji wanashauriwa kuitumia kwa uangalifu kutokana na hali ya unyeshaji wa mvua usioridhisha katika maeneo mengi nchini.